Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 6.

Teknolojia imeleta mfumo mpya wa maisha kote ulimwenguni. Imekuwa nadra sana kwa watu wa mataifa kutekeleza kazi zao kivyao. Hii ni kwa sababu mitambo ya tarakilishi imeenea kote na matumizi yake si mapya tena. Hali hii imekuwa msukumo mpya wa maendeleo katika nyanja mbalimbali za nchi kama vile biashara, uvumbuzi wa bidhaa mpya viwandani na vyombo vya kuonewa fahari katika makazi ya watu vikiwemo redio, runinga na majiko.

Kweli dunia nzima imekuwa kijiji tu, mlango wa kwenu unakabiliana na wa kwetu na mawasiliano, mapatano na uhusiano huo huwa bayana zaidi. Kale, watu walichukua muda mrefu kuandikiana nyaraka zilizochukua miezi kadhaa kufika; siku hizi huduma hii ya shirika la posta na nyingine hapa na pale si kizuizi kikubwa kwa mawasiliano na umuhimu wake umeachiwa uwasilishi wa vifurushi. Watu wengi hutuma ujumbe mfupi kwa rununu. Baruapepe nazo ni nyingine ambazo zimeimarisha mawasiliano hasa kutoka mabara; pasi kuwa na gharama kuu kama hapo awali. Kipepesi na mitambo ya umeme vinatumika katika nyanja mbalimbali kote duniani.

Hata hivyo, kila masika yana mbu, nao mbu husambaza malaria. Kupitia vyombo vya habari na mawasiliano, vijana wetu wamechukua hulka za Kizungu. Matumizi ya dawa za kulevya, kujivalia nusu uchi na lugha chafu ni baadhi ya mambo yanayochangia ongezeko la visa vya ubakaji.

Ni kweli kuwa mambo mapya yakija watu hujifunza mengi lakini si yote ambayo huja yana manufaa.

1. Watu wa mataifa hawawezi kutekeleza shughuli kivyao kwa sababu
A. mawasiliano yamekuwa ya gharama kuu.
B. ulimwengu umekuwa kijiji tu.
C. kiwango cha teknolojia kimekuwa sawa kote.
D. mataifa mengi hayana nguvu za umeme.

2. Neno **nadra** kama lilivyotumika katika kifungu linamaanisha
A. kawaida B. muhali
C. mbeleni D. rahisi

3. Ni jambo gani limechangia kuunganisha ulimwengu wa sasa?
A. Masomo ya sayansi.
B. Ueneaji wa nguvu za umeme.
C. Uuzaji wa dawa za kulevya.
D. Mawasiliano.

4. Baruapepe hutumika nyakati hizi kwa sababu zifuatazo isipokuwa
A. zina gharama ya chini.
B. huchukua muda mfupi kuwasilisha ujumbe.
C. uvumbuzi wa teknolojia mpya.
D. watu wote duniani wana elimu ya teknolojia.

5. Kulingana na kifungu, matumizi ya mihadarati yanaongeza visa vya
A. ubakaji B. wizi
C. usalama D. mauaji

6. Kasoro moja ya teknolojia ni
A. kuwaelimisha watu.
B. kutangaza habari za ulimwengu
C. watu kupoteza maadili ya kiasili na kuiga za kigeni.
D. kueneza habari duniani kote.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 7 hadi la 12.

Ni jambo lisilopingika kuwa, elimu ni ufunguo wa maisha. Aidha, elimu ni nguzo imara ya kuegemea maishani. Hata hivyo, yafaa ifahamike kuwa elimu itamfaidi mmiliki wayo yule ambaye anaitumia kwa ufasaha. La muhimu zaidi, yule ambaye ataitumia kwa nidhamu, hekima na heshima.

Haijalishi iwapo mtu amesoma matopa ya vitabu. Haijalishi amefikia kiwango kipi au anazo shahada zipi: Iwapo hana adabu, heshima, nidhamu na awajibikaji, elimu yake haijakamilika. Elimu hiyo si lolote si chochote. Elimu yake itakuwa kama pambo haliwezi kusitiri mtu. Hiyo ni kazi ya nguo.

Ni fedheha kuwaona baadhi ya watu wakichachawiza kuwa wameelimika ilhali wenzao ni fuska. Heshima kwao ni mwiko. Adabu kwao ni neno geni. Ukweli ni kuwa elimu hiyo yao haina faida kwa walimwengu. Mwalimu wangu wa zamani alinieleza kuwa kumiliki elimu ya aina hiyo ni sawa na kufunga tai huku mtu akiwa uchi wa mnyama.

Ni jambo aula mtu kuonyesha elimu yake kwa vitendo. Vitendo vya yeyote aliye na elimu vinafaa viwe na mwelekeo na vya kutamanika. Vionyeshe ustaarabu wala si ushenzi. Aidha, ifahamike kuwa elimu si ya vitabu tu. La hasha! Ipo pia elimu ya dunia. Sharti elimu yetu ituwezeshe kutafakari ya dunia.